**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**MALALAMIKO NAMBA. GA.71/472/CZ/2024/08**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000170**

**KATI YA**

**SALIM MKUMBA ………………………………………………………… MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI**
**WA MAZINGIRA MOROGORO**
**(MORUWASA) ………………………………………………………… MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 144 cha tarehe 17 mwezi Januari 2025)***

## 1.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 02 Julai 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Salim Mkumba akiwakilishwa na Bw. David Nzota wa S. L. P. 40 Morogoro, Kilakala Sekondari, Mkoa wa Morogoro (Mlalamikaji) dhidi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa

Mazingira Morogoro ("MORUWASA") (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumtoza ankara za maji safi zisizolingana na matumizi yake katika eneo analoishi, la kiasi cha Shilingi 913,040/= ikiwa ni ankara ya mwezi Aprili 2022.

Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba alichukua hatua mbalimbali ikiwemo kwenda ofisini kwa Mlalamikiwa ambapo Mlalamikiwa aliahidi kutatua changamoto hiyo lakini baada ya hapo, hakukuwa na suluhu yeyote ya tatizo hilo. Mlalamikaji aliandika barua kwenda kwa Mlalamikiwa tarehe 12/07/2022 ambapo barua hiyo ilijibiwa tarehe 22/02/2023 lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Hivyo basi, Mlalamikaji anaiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kurekebisha ankara hiyo ya shilingi 913,040/= ili aweze kulipa kiasi halali cha ankara anayotakiwa kinachoendana na ankara zao wanazolipa kila mwezi.

Baada ya kupokea malalamiko ya Bw. Said Mkumba tarehe 09 Julai 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020)) TS Na. 428/2020.

Mnamo tarehe 25 Julai 2024, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kuieleza Mamlaka kwamba anakiri kupokea malalamiko haya na ameeleza kwamba Mlalamikiwa aliwaagiza mafundi wake kwenda kwa Mlalamikaji na kufanya uchunguzi wa mambo matatu ambayo ni kuhakiki usomaji wa dira, kukagua mvujo mbele ya dira ya maji na kupima ufanisi wa dira ya maji .

Baada ya uchunguzi huo ilibainika kuwa eneo la Mlalamikaji kulikuwa na mvujo mbele ya dira ya maji katika mojawapo ya nyumba zinazotumia dira hiyo na Mlalamikaji kuelezwa kuwa suala la mvujo mbele ya dira yake ndio chanzo cha ankara kubwa, lakini alishindwa kuelewa. Hivyo, ankara hiyo Mlalamikaji

anapaswa kuilipa kwani hana utaratibu wa kuondoa deni la ankara inayotokana na mvujo mbele ya dira ya Mteja (Mlalamikaji).

Vikao vya usuluhishi baina ya pande zote mbili vilifanyika tarehe 21 Agosti 2024, 21 Oktoba 2024 na 02 Januari 2025 katika ukumbi wa Aika Hotel uliopo Morogoro Mjini, Mkoa wa Morogoro.

Mwisho wa kikao cha usuluhishi tarehe 02 Januari 2025, muafaka ulifikiwa kwa makubaliano yafuatayo:-

(i) Kwamba Mlalamikaji atalipa deni la ankara ya TZS 215,824.44 badala ya deni la ankara ya TZS 913,040/= ambazo alikuwa akidaiwa awali; na

(ii) Mlalamikaji atalipa deni hilo la TZS 215,824.44 kwa kipindi cha miezi minne kuanzia leo tarehe 02 Januari 2025 kwa kiasi cha TZS 53,956.11/= hadi tarehe 30 Aprili 2025.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali Na. 428 la 2020 na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kuwa Mlalamikiwa atalipa deni la ankara ya TZS 215,824.44 badala ya ankara ya TZS 913,040/= ambazo alikuwa akidaiwa awali na Mlalamikiwa amekubali Mlalamikaji kulipa deni hilo la TZS 215,824.44/= kwa kipindi cha miezi minne kuanzia leo tarehe 02/01/2025 kwa kiasi cha TZS 53,956.11 hadi tarehe 30/04/2025.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande

itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Dodoma tarehe 17 mwezi Januari 2025.

..................................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**